EAST AFRICA LEGISLATIVE ASSEMBLY

KAKAMA YAANZA MAFUNZO YA KISWAHILI KWA WAJUMBE WA BUNGE LA AFRIKA MASHARIKI

Taarifa kwa Vyombo vya Habari

Arusha, Tanzania- Novemba, 26th, 2026- Kamisheni ya Kiswahili ya Afrika Mashariki (KAKAMA) imetamatisha programu ya mafunzo ya Kiswahili kwa Wajumbe wa Bunge la Afrika Mashariki (EALA). Mafunzo haya yamekuwa **yakiendelea** katika **makao makuu ya** Sekretarieti ya Jumuiya ya Afrika Mashariki (JAM), jijini Arusha, kuanzia tarehe 23 hadi 25 Novemba, 2026.

Wakati wa kufungua mafunzo hayo, Mheshimiwa Dkt. Abdullah Makame, Mwenyekiti wa Kamati ya Masuala ya Mtambuka ya EALA, aliwashukuru KAKAMA kwa kuandaa mafunzo hayo kwa ajili ya Wajumbe wa Bunge la Afrika Mashariki. Alisisitiza kuwa, kwa kuwa wajumbe hao ni wawakilishi wa wananchi wa Jumuiya ya Afrika Mashariki, ni muhimu kujifunza Kiswahili ili waweze kushirikiana na wananchi wengine na kutekeleza majukumu yao kwa kutumia lugha ya Kiswahili. Alisisitiza kwamba umahiri wa Kiswahili unaimarisha uwezo wa Wajumbe kutekeleza majukumu makuu ya Bunge, ambayo ni kutunga sheria, kusimamia utekelezaji wa shughuli za Jumuiya na kuwawakilisha wananchi. Kupitia Kiswahili, Wajumbe wanaweza kuwasiliana moja kwa moja zaidi na wananchi, kushiriki kikamilifu katika mijadala ya kikanda na kuchangia kwa ufanisi zaidi katika mijadala inayounda mustakabali wa Jumuiya yetu. Alibainisha kuwa mafunzo hayo ni sehemu ya programu ya ushirikiano kati ya Bunge na Kamisheni, inayolenga kuimarisha umahiri wa Wajumbe katika lugha ya Kiswahili kupitia programu ya mafunzo iliyoandaliwa kwa utaratibu maalumu.

Dkt. Caroline Asiimwe, Katibu Mtendaji wa KAKAMA, alibainisha nafasi muhimu ya Wajumbe wa Bunge la Afrika Mashariki katika kuimarisha ushirikiano na utangamano wa kikanda, pamoja na umuhimu wa Kiswahili katika utekelezaji wa majukumu yao. Alibainisha kuwa, mbali na kuwa lugha inayotumika kwa mawasiliano mapana katika Jumuiya ya Afrika Mashariki, Kiswahili pia kimepitishwa kuwa mojawapo ya lugha rasmi za JAM na kinaendelea kupata nafasi kubwa duniani. Aligusia kuwa mafunzo hayo ni hatua muhimu katika kuifanya lugha ya Kiswahili ionekane zaidi na itumike katika shughuli za kila siku za utawala wa kikanda. Tunaamini kwamba Wabunge wanapokithamini, kukielewa, kukizungumza na kukitumia Kiswahili kwa kujiamini, wanakuwa katika nafasi nzuri zaidi ya kuwasiliana na wananchi, kueleza vipaumbele vya kikanda na kuimarisha utambulisho wa Afrika Mashariki.

Kwa msingi huo, KAKAMA wameanza na Bunge la Afrika Mashariki katika kutekeleza programu ya kujenga uwezo wa vyombo na taasisi za JAM katika matumizi ya Kiswahili. Wa Wabunge watashiriki katika shughuli mbalimbali za kujifunza lugha hiyo. Baada ya mafunzo ya ana kwa ana

yanayofanyika katika Makao Makuu ya JAM, Arusha, mafunzo wataendelea mtandaoni kwa utaratibu utakaowawezesha washirki kutimiza mahitaji ya kuhitimu kozi hiyo. Kuimarika kwa uwezo wa kutumia Kiswahili kutasaidia kupunguza vikwazo vya lugha Bungeni, kukuza ushirikishwaji na kuimarisha nafasi ya Bunge la Afrika Mashariki kama taasisi ya kikanda inayowakilisha na kuwasiliana na wananchi wa Afrika Mashariki. Aidha, hatua hiyo inaunga mkono lengo pana la kukijumuisha Kiswahili kikamilifu katika taasisi za kikanda na kuimarisha utambulisho wa kitamaduni na kilugha unaowezesha utangamano wa kikanda.

Dkt. Obatre, Katibu wa Bunge la Afrika Mashariki, alitambua nafasi muhimu ya Wajumbe wa Bunge la Afrika Mashariki kujifunza Kiswahili ili waweze kutekeleza majukumu yao kwa ufanisi zaidi na kuwasiliana vizuri na wananchi wa kawaida wa Nchi Wanachama za Jumuiya ya Afrika Mashariki.

Programu hiyo inatekelezwa kwa kushirikiana na MS TCDC iliyopo Arusha, ambayo ni mshirika muhimu katika kujenga uwezo na kuwezesha mafunzo ya vitendo. Baadhi ya vipindi pia vinaendeshwa na wawezeshaji kutoka taasisi nyingine zinazoshirikiana na KAKAMA katika utekelezaji wa shughuli za kukuzxa na kuendeleza Kiswahili.

Kwa Maelezo Zaidi, Wasiliana na:

Nicodemus Ajak Bior
Senior Public Relations Officer (SPRO)
East Africa Legislative Assembly
Arusha, Tanzania
Tel: +255-768-885-633/, +254729157207(WhatsApp)
Email: nbior@eachq.org
Web: www.eala.org